**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents Government Budget Speeches

1987-05

# Hotuba ya Rais Ally Hassan Mwinyi 1987,kuhusu Hali ya Uchumu Wetu

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/664

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

# HOTUBA YA RAIS
# ALI HASSAN MWINYI



## HALI YA UCHUMI WETU

*Iringa,* *Mei 1, 1987*

# HOTUBA YA RAIS ALI HASSAN MWINYI KWENYE SIKUKUU YA WAFANYAKAZI (MAY DAY), IRINGA. 1/5/87

Ndugu Viongozi wa Chama na Serikali,
Ndugu Wafanyakazi,
Ndugu Wananchi.

Kwanza kabisa napenda kutumia nafasi hii kutoa shukrani zangu kwa Viongozi wa Mkoa wa Iringa na Viongozi wa Juwata kwa kunialika mimi mfanyakazi mwenzenu kujumuika nanyi, hapa Iringa, katika sherehe za mwaka huu za kuadhimisha siku ya wafanyakazi Duniani. Pili napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wananchi wote wa Mkoa wa Iringa kwa ukarimu wao wa kukubali kuwa wenyeji wa sherehe hizi. Sote tunatambua kwamba maandalizi ya sherehe kama hii huwa ni mzigo mzito kwa wahusika. Hapana shaka mazuri yote yaliyojitokeza hapa ni matokeo ya kazi ngumu ya kupanga na kutekeleza. Ni wazi kabisa kwamba mafanikio haya ni matunda ya jasho, uvumilivu na ushirikiano kati ya viongozi na wananchi. Sina shaka kuwa hiyo ndiyo siri iliyokuwezesheni, kutupa sisi sote, wageni wenu, mapokezi ya kidugu na makaribisho mazuri.

Pia, ningependa kutumia nafasi hii kuwapa hongera wafanyakazi wote waliotunukiwa zawadi mbali mbali hii leo kwa kuchomoza katika utendaji mwema wa kazi katika mwahali mwao mwa kazi. Nawapa hongera kwa niaba ya Chama, Serikali, Juwata na wananchi. Matumaini ya Taifa ni kwamba nyinyi wenzetu mliopewa zawadi hii leo si visiwa katika bahari ya wavivu bali ni vilele kwenye milima ya wafanyakazi wazuri. Hamko peke yenu bali nyinyi ndio mliochomoza. Tunajua zawadi mlizopewa siyo kipimo cha uzuri wa kazi zenu. Zawadi hizo ni ishara tu au kitambulisho kwamba Taifa linakiri hadharani jinsi linavyothamini mchango wenu.

Matarajio yetu ni kwamba mtakuwa kama maua ya waridi mwahali mwenu mwa kazi, hamtanukia peke yenu, bali hata wale walio karibu nanyi mtawaambukiza harufu nzuri.

Kwa maneno mengine ni kwamba ushindi wenu utakuwa ni changamoto kwa wale wafanyakazi wengine ambao utendaji wao wa kazi bado haujaridhisha. Maana ijapokuwa kwa jumla ufanisi katika utendaji kazi umeongezeka nchini, bado wapo wafanyakazi wachache wanaoturudisha nyuma. Ni wajibu wenu ninyi wafanyakazi bora wa leo, kwa kushirikiana na wafanyakazi wengine wazuri, kuwahamasisha na kuwaelekeza wale wenzetu wanaovuruga sifa yetu ili wajirekebishe. Tusiwaruhusu wachache kurudisha nyuma juhudi za wengi, katika wimbi tulilolianzisha la kufufua na kuimarisha uchumi wetu. Kwa hiyo siku hii ya leo ni wakati mzuri wa kutoa maazimio ya kuchapa kazi zaidi na kubuni mikakati ya kuongeza uzalishaji mali kwa mwaka unaoanza sasa. Tunaweza kuyatekeleza hayo kwa kugawana kazi na kwa kila mmoja wetu kutekeleza wajibu wake mahali alipo kwa ukamilifu.

Na mwisho, ningependa kuupongeza uongozi mzuri wa Juwata kwa kazi njema walioifanya katika miezi kumi na miwili iliyopita tokea kuachana katika sherehe kama hii mwaka jana. Kumekuwa na matatizo mengi kidogo ya wanachama, na wameyakabili matatizo kwa ushujaa, uadilifu na uzalendo—bila ya kujipendekeza kwa waajiri wala kwa wafanyakazi waliokuwa na hatia. Mwendo huu mzuri ni lazima tuudumishe.

Ndugu Wananchi, sherehe hizi zinafanyika siku nne tu baada ya sherehe za miaka 23 ya Muungano wetu. Katika muda wote huo uhuru wetu na umoja wetu umekuwa ukiimarika. Tofauti za utekelezaji zinapochomoza, tumekuwa tukizikabili kwa mazungumzo na maelewano ya kidugu. Lakini wakati sisi wafanyakazi wa Tanzania tunajivunia umoja na uhuru wetu, inafaa tukumbuke kwamba wapo

wafanyakazi wenzetu, na ndugu zetu, huko Afrika ya Kusini ambao sherehe za namna hii kwao ni ndoto tu— kwani bado wanaendelea kunyonywa, kuteswa, kunyanyaswa na kuuliwa ovyo na Makaburu. Yaliyowafika COSATA majuzi mmeyasikia. Kosa lao kubwa hata wakalazimika kukutwa na janga hilo ati ni kwa kuwa weusi!! Katika siasa haramu ya ubaguzi, kwa misingi ya rangi, inayoendeshwa na makaburu, watu weusi hawana haki za kiraia huko Afrika ya Kusini.

Ukiwa mweusi huruhusiwi kupiga kura wala kushiriki katika kuwachagua viongozi wa nchi yako. Unanyimwa haki hata ya kutetea maslahi yako. Wafanyakazi wenzetu huko Afrika ya Kusini wamekosa hadhi hata zile wanazozipata watumwa kwa bwana zao. Kwani watumwa huweza kuruhusiwa kulala ndani ya nyumba za bwana zao baada ya kazi. Waafrika huko Afrika ya Kusini hawathubutu kufanya hivyo. Jua likitua lazima watoke mbio katika mitaa au majumba ya weupe wanaowahudumia; anayechelewa, huuawa kama kuku. Huko Afrika ya Kusini mtu mweusi hana hadhi ya utu. Yeye huwa ni mfano wa chombo tu cha kutumiwa na weupe ili kuwapatia, weupe hao, mali na huduma. Waafrika wanaokataa hayo, na wale wanaopinga ubaguzi wa rangi, hutendewa vitendo viovu vya kinyama.

Lakini inatia moyo kujua kwamba sasa wazalendo wa Afrika ya Kusini wamechoka kuonewa. Wamepiga "kifua konde" na kusema potelea mbali!! Wameamua kupambana na makaburu ili kufuta utaratibu wa ubaguzi wa rangi na kurejesha haki na heshima ya Waafrika, bila kujali maisha yao. Idadi ya wazalendo wanaopoteza maisha yao inazidi kuongezeka. Hawajali. Upinzani wao sasa umepamba moto kweli kweli. Kwa sababu hiyo, Makaburu wameanza kufadhaika na kutapatapa. Katika fadhaa yao wanazidisha vitendo vyao vya kikatili na kinyama dhidi ya wazalendo.

Lakini tunaamini kabisa kwamba mwishowe wazalendo watashinda. Maana historia inatudhihirishia kwamba dhuluma siku zote haiwezi kushindana na haki. Penye mapambano kati ya haki na dhuluma, siku zote haki hushinda. Makaburu wanataka kudumisha dhuluma kwa manufaa yao. Lakini ni wazi kabisa hawataweza kufaulu hata wakitumia nguvu zao zote. Wazalendo wanaotetea haki lazima watashinda. Huko Namibia pia wazalendo wameongeza mapambano dhidi ya utawala dhalimu wa Makaburu. Wananchi wa Namibia nao pia watashinda maana wanatetea haki na uhuru wao.

Ndugu Wananchi,

Historia ya Watanzania ya kuwasaidia wenzao wanaopigana kwa kutetea haki na uhuru wao, haihitaji maelezo mengi. Napenda kusisitiza tu kwamba siasa ya Chama chetu—ambacho ni Chama cha Ukombozi—na Serikali yake, siku zote, ni kutetea haki za wanyonge, ndani na nje ya Tanzania, pamoja na kuunga mkono harakati za kupigania uhuru. Kutokana na msimamo huo, Tanzania itaendelea kuwaunga mkono Wazalendo wa Afrika ya Kusini na wa Namibia mpaka watakapojikomboa na kuhakikisha kwamba sheria ya ubaguzi wa rangi inafutwa.

Tunafanya hivyo kwa kutambua kwamba, kuendelea kuwapo kwa siasa za ubaguzi, ni tishio kubwa kwa amani katika eneo lote la Kusini mwa Afrika. Ni tishio vile vile kwa uhuru wa nchi yetu, na nchi jirani za mstari wa mbele. Sote tunafahamu shida kubwa wanayopata wenzetu wa Msumbiji kutokana na vitendo vya uchokozi vinavyofanywa na Makaburu kwa kuwatumia mamluki wao wanaojiita Renamo. Nia ya Serikali ya Makaburu ni kuziangusha Serikalli za nchi za Mstari wa Mbele ili waweke vibaraka wao watakaounga mkono siasa zao za ubaguzi wa rangi. Wakifanikiwa kufanya hivyo huko Msumbiji, tutajikuta tunapakana na Makaburu hapa petu.

Kwa hiyo, kwetu sisi ni jambo la msingi kabisa kuendelea kuwasaidia wenzetu wa Msumbiji kwa hali na mali, ili waweze kuwashinda magaidi wa Renamo, na kuimarisha uhuru wao. Hii ndio sababu Tanzania imeanzisha mfuko maalum wa kuwasaidia ndugu zetu wa Msumbiji. Napenda kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya Chama na Serikali, na kwa niaba yangu mimi mwenyewe, kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wote kwa michango yao, ya utu na kitu, katika kuwasaidia ndugu zetu wa Msumbiji.

Tutaendelea pia kuyashawishi mataifa mengine duniani, hasa yale yanayoshirikiana na makaburu, kuacha kufanya hivyo, na badala yake kuongeza juhudi za kuubana utawala huo ili ubadilishe siasa zake za ubaguzi. Njia pekee iliyobakia ya kuleta mabadiliko kwa amani huko Afrika ya Kusini ni kuuwekea utawala huo vikwazo vya uchumi. Kwa hiyo matumaini yetu ni kwamba Jumuia ya Kimataifa mwishowe itakubaliana nasi katika kuiwekea Serikali ya Afrika ya Kusini vikwazo vya uchumi.

Ndugu Wananchi, yafaa tukumbuke kwamba maonevu hayako Afrika ya Kusini tu. Huko Mashariki ya Kati kunatendeka maonevu na dhuluma zinazofanana na zile zinazotendeka Afrika ya Kusini. Kuna wenzetu wa Palestina ambao nao pia wanatendewa maovu na Serikali ya Israeli. Wakati Waafrika wa Afrika Kusini wanaonewa hali wapo kwao, Wapalestina hawana hata mahali wanapoweza kupaita kwao. Wamepokonywa ardhi yao. Sasa wamekuwa kama ndege waliokatiwa mti wao. Wamesambaa tu, hawana mahali pa kutua!

Tanzania itaendelea kuwaunga mkono wenzetu hao Wapalestina katika mapambano yao ya kudai haki ya kujiamulia mambo yao na kupata nchi yao wenyewe.

Ndugu Wafanyakazi na Ndugu Wananchi,

Mei, Mosi, husherehekewa mara moja tu katika mwaka. Hivyo basi siku ya kuadhimisha sherehe hiyo inapofika, huwa ni wakati mzuri wa kukaa chini na

kutafakari kwa makini sana utendaji wetu wa kazi kwa kipindi kizima cha mwaka uliopita. Nashauri tuanze kufanya hivyo mwaka huu. Tujipe nafasi ya kutathmini mafanikio yetu na matatizo tuliyopambana nayo tokea tulipoachana baada ya sherehe za mwaka jana. Inafaa pia tutumie nafasi hii kujikumbusha kasoro zetu na wajibu wetu katika utendaji wetu wa kazi na kutafakari jinsi ya kuongeza ufanisi na tija katika sehemu zetu za kazi. Madhumuni yetu yawe ni kujifunza kutokana na makosa yetu na kuimarisha mbinu zilizotuletea mafanikio. Risala iliyosomwa na Katibu Mkuu wa JUWATA imeyataja baadhi ya mambo hayo. Mengine yamesemwa na Mwenyekiti wa JUWATA katika hotuba yake aliyoitoa hivi punde. Hivyo, si nia yangu kukuchosheni kwa kuyarudia. Lakini pengine ni vizuri nichukue nafasi hii kusisitiza tu, baadhi ya yale mambo yanayohitaji kusisitizwa, ingawa si mageni kwetu.

Ndugu Wafanyakazi,

Sherehe hizi mwaka jana zilifanyika katika mazingira magumu sana ya hali mbaya ya uchumi. Hali hiyo bado haijatengenea. Mwaka jana tulikuwa na uhaba mkubwa wa bidhaa za viwandani kama vile sabuni, dawa za mswaki, nguo, mafuta ya taa na vifaa mbali mbali vya ujenzi.

Mwaka huu haijambo kidogo, lakini bado hali si ya kuridhisha. Vyakula kama mchele, ngano na sukari pia vilikuwa vikipatikana kwa shida mwakajana, hasa katika miji kama vile Dar es Salaam. Wakati mwingine hata mahindi yalikosekana mijini; na si kwamba hayakuwapo hapa nchini, yalikuwapo, bali tulishindwa kuyasomba na kuyasambaza hadi kuwafikia walaji, kwa sababu, vyombo vya uchukuzi vilikosa mahitaji yake kama vile mipira, deseli, petroli na spea. Mwaka huu hali si mbaya kiasi hicho, lakini bado hatujaondokana na matatizo.

Kutokana na hali hiyo, bei zimekuwa zikipanda kupita kiasi. Uwezo wa Watanzania wengi, na hasa wafanyakazi, wa kujinunulia mahitaji muhimu kwa maisha yao, umepungua sana kwa sababu ya ongezeko la bei. Hali ya maisha, hasa mwaka jana, iliendelea kuwa ngumu hata baada ya Serikali kutoa posho kwa wafanyakazi wanaotegemea mishahara. Kwa bahati mbaya posho iliyotolewa, kwa nia njema kabisa ya kuwapunguzia wafanyakazi uzito wa kukabili maisha, ilionekana kama ni kichocheo cha kuongezeka kwa bei. Kwani kila mwenye chake alipandisha bei kana kwamba asionekane ameshindwa katika mashindano ya kuuza ghali (kuongeza bei).

Kwa hiyo napenda kuchukua nafasi hii kukupeni pole kwa matatizo mliyoendelea kupambana nayo kwa kipindi chote cha mwaka mzima. Mnachostahiki ni kupongezwa kwa kuendelea kufanya kazi kwa uvumilivu, utulivu na amani katika mazingira magumu. Ningependa kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya Chama na Serikali, na kwa niaba yangu mimi binafsi, kukushukuruni sana kwa kuyakabili matatizo hayo kwa moyo wa kizalendo.

Matatizo haya yamekuwapo kwa zaidi ya miaka sita sasa. Sababu zilizotufikisha katika hali hii tunazielewa. Lakini si vibaya kukumbushana, kila tunapokutana, zile sababu kubwa za kuzorota kwa uchumi wetu, nazo ni kushuka kwa kilimo cha mazao ya chakula na biashara. Mtanisamehe kurudia rudia mifano niliyokwisha kukariri mara nyingi tunapokutana, nayo ni kwamba mavuno yetu kwa kipindi kirefu yamekuwa yakipungua, mfano:

— Pamba tunayolima imepungua kutoka tani 57,151 mwaka 1981 hadi tani 36,000 mwaka 1985/86.
— Katani imepungua toka tani 230,000 katika miaka ya 60 hadi tani 32,000 mwaka 1985/86.
— Korosho imeshuka kutoka tani 145,000 mwaka 1973, hadi tani 17,200 mwaka 1985/86.

Hii ndiyo hali ya mazao ya biashara. Hali ya kilimo cha mazao ya chakula haikutofautiana na hii ya mavuno ya biashara.

Takwimu zifuatazo zinadhihirisha ukweli huo. Kwa mfano:—

— Mahindi yamcterernka kutoka tani 222,500 mwaka 1978 hadi tani 89,000 mwaka 1984/85.
— Mpunga umeshuka kutoka tani 60,800 mwaka 1971 hadi tani 23,000 tu. mwaka 1985/86.

Kushuka kwa kilimo cha mazao ya chakula kumeilazimu Serikali kuagiza chakula kwa pesa za kigeni kutoka nje kufidia upungufu uliopo. Mfano:—

| | *1982/83* | *1983/84* | *1984/85* | *1985/86* |
|---|---|---|---|---|
| Mahindi tani ............ | 122,600 | 231,100 | 234,700 | 25,600 |
| Mchele tani .............. | 29,400 | 58,900 | 46,500 | 39,600 |
| Nganotani ............... | 11,900 | 37,400 | 35,600 | 14,100 |
| Jumla tani ... | 163,900 | 327,400 | 316,800 | 79,300 |

Kulazimika kuagiza chakula, matokeo yake yanafanana na ule usemi wa Biblia kwamba hata kile kidogo tulichokuwa nacho (katika fedha za kigeni) tulinyang'anywa ili kuongezewa waliokuwa nacho. Hili ni tatizo. Na ni mojawapo ya sababu zinazochangia hali mbaya ya uchumi wetu.

Sote tunafahamu kwamba mazao ya biashara ndio chemchem zinazotupatia fedha za kigeni. Fedha hizo ndizo zinazotumika kuagiza mafuta, malighafi na spea kwa matumizi ya viwanda vyetu. Kwa hiyo kushuka kwa kilimo cha mazao ya biashara kunalipunguzia Taifa mapato yake. Matokeo yake sote tunayajua. Viwanda vyetu vingi hivi sasa vinasindika chini ya asilimia 30 ya uwezo wao kutokana na ukosefu wa malighafi na spea. Hii ndio sababu tunao upungufu mkubwa wa bidhaa za viwandani.

Kwakuwa tunalazimika kutumia mapato yetu ya fedha za kigeni kununulia chakula, kiasi cha fedha kinachosalia, baada ya kununua chakula, kinashindwa kukidhi mahitaji yetu mengine. Tumekuwa ni Taifa la wachumia tumbo. Matokeo yake ni kwamba mapato yetu hayalingani kabisa na matumizi yetu.

Na kwa kuwa Taifa linakua, na idadi ya watu inaongezeka, matumizi yetu yamekuwa yakiongezeka vile vile mwaka hadi mwaka, na huku mapato yetu yamekuwa yakipungua mwaka hadi mwaka, badala ya kuongezeka kulingana na ongezeko la watu. Matokeo yake ni kwamba tunayo madeni makubwa ambayo kuyalipa kwake kunatupa shida. Kwa hiyo hatuwezi kuendelea kukopa bila ya kufanya juhudi za kuongeza mapato yetu wenyewe. Pia, tusidhani kwamba tutaendelea kukopeshwa baada ya kugunduliwa kuwa hatuna uwezo wa kulipa.

Kutokana na hali hiyo, ni dhahiri kwamba njia kubwa ya kutupunguzia matatizo yetu ni kuongeza kilimo cha mazao ya chakula na ya biashara pamoja na kuongeza wingi wa bidhaa za viwandani. Uwezo wa kuongeza mazao ya kilimo tunao. Tunachopaswa kufanya ni kuongeza juhudi, maarifa na ufanisi katika kilimo, viwanda na kila mahali pa kazi. Ndio maana nimesisitiza mara nyingi umuhimu wa kila mmoja wetu kuwajibika mahali pake pa kazi. Wito huo umeitikiwa vizuri na wananchi na matunda yake yameanza kuonekana pole pole.

Hapa ninafurahi kusema kwamba zipo dalili nzuri zinazoonyesha kwamba wananchi wameongeza juhudi katika kuwajibika. Dalili hizo zinaonekana wazi wazi zaidi katika kilimo. Kutokana na juhudi za wakulima, uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara umeongezeka kwa kiasi kikubwa mwaka huu. Hivi sasa tunazo zaidi ya tani laki mbili za mahindi katika ghala la Shirika la Usagishaji. Hii ni ziada baada ya wakulima kujiwekea akiba yao ya chakula. Pia tunayo maharagwe



**Rais Ali Hassan Mwinyi akihutubia Taifa wakati**
**kwenye uwanja wa**

# HONGERA MWALIMU



*Dodoma,* *Septemba 7, 1987*